



---

## **MAKALA YA AFYA / HEALTH PUBLICATION**

### **AFYA YA UZAZI/REPRODUCTIVE HEALTH**

#### **KUTOPATA MIMBA/UJAUZITO (INFERTILITY)**

Ujauzito ni hatua kubwa na muhimu katika Maisha. Kwa baadhi ya wanandoa au watu walio kwenye mahusiano, kupata ujauzito hutokea bila tatizo lolote lakini kwa baadhi inahitaji kuwa na uvumilivu na bahati.

Iwapo umefikia umri wa kupata ujauzito ni vizuri kuzingatia baadhi ya mambo kama vile kuwa na uzito unaofaa, kutokunywa pombe kwa wingi na kutokuvua sigara kwa wanawake na wanaume pia.

Watu walio wengi ambao wako kwenye mahusiano na wanashiriki tendo la ndoa, ujauzito hupatikana ndani ya mwaka mmoja. Endapo ujauzito umechelewa zaidi ya hapo, ni vizuri kumuona mtaalamu wa afya ili aweze kutoa ushauri. Hata hivyo kwa baadhi ya watu, hasa kama mwanamke ana umri zaidi ya miaka 35, au kuna matatizo yoyote ya kiafya ni vema kumuona madaktari mapema zaidi.

Matatizo mengi ya kukosa kupata ujauzito hutibika endapo tatizo litagundulika mapema. Hivyo ni vizuri wote wawili kuonana na madaktari bingwa wa magonjwa ya uzazi ili kuweza kugundua tatizo na kupata tiba.

Baada ya kugundua chanzo cha kutopata ujauzito, mtaalamu wa afya atashauri tiba stahiki. Tiba inaweza kuwa ushauri wa siku za kukutana kimwili. Tiba nyingine inategemea na tatizo lililogundulika na matibabu yanaweza kuwa vidonge au sindano za kupevusha mayai au kuongeza mbegu za kuime; upasuaji wa mirija iliyoziba kwa ajili ya kupitisha mayai, upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye mfuko wa uzazi, kuasabisha yai na mbegu kushindwa kukutana au mimba kushindwa kupandikizwa kwenye mfuko wa uzazi. Maendeleo katika sayansi ya afya yamewezesha upandikizaji wa mbegu za kiume au kupandikiza mimba iliyotungwa kwenye maabara kwenye mfuko wa uzazi wa mwanamke kwa kutumia mbegu na yai la wahusika. Teknolojia hii inaweza kusaidia wale ambayo mirija haiwezi kupitisha mbegu au yai.

*Na Madaktari bingwa wa magonjwa ya Homoni na Uzazi – HM Hospital - Bunju B*

***Kwa Huduma ya Kuonana na Daktari Bingwa piga simu namba:***

***+255 748 053303/+255 754 587900/+255 755 085586***